



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA ILEJE



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HWI/20/1/42

16 Februari, 2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA KUKUSANYA TAARIFA ZA
ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Ileje anapenda kuwatangazia Nafasi za ajira ya muda kwa nafasi za wakusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za Makazi katika kata na Vijiji vya Wilaya ya Ileje.

A. SIFA ZA WAOMBAJI

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35.
- ii. Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- iii. Awe anamiliki simu Janja Android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima.
- iv. Awe na barua pepe(email address) na nywila (password) inayofanya kazi.
- v. Awe na uwezo wa kusoma ramani za vijiji.
- vi. Awe ni mkazi wa Kata husika.

B. KAZI NA MAJUKUMU

- a) Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.
- b) Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma.

- c) Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa anwani za makazi.
d) Kutuma data kwenye mfumo wa anwani za makazi,

MALIPO: Malipo yatafanyika kwa kiasi cha kazi kwa siku.

C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA;

1. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea,
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa,
3. Picha (passport size 2),
4. Barua ya maombi ipite kwa mtendaji wa kijiji na Kata anapoishi.

D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI


Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, namba ya simu na barua pepe na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri kwa Anwani ifuatayo.

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI
S.L.P 02
ILEJE**

E. TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 23/02/2022 saa 9.30 alasiri.

Tangazo hili limetolewa na; -


Pastory M. Mashiku.

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S. L. P. 2**

ILEJE

Halmashauri ya Wilaya ya Ileje, S.L.P 2, Ileje - Songwe, Simu +025-2570050 +025-2570050, Nukushi +255 025-2570143, Barua pepe: ded@ilejedc.go.tz , Tovuti: www.ilejedcdc.go.tz